**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

**TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)**

# MWONGOZO WA TAMASHA LA KIMATAIFA LA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO, 2023

## MWONGOZO WA TAMASHA

*(Umeandaliwa chini ya Aya 3, aya ndogo ya 3.5 ya Jedwali la Sheria iliyoanzisha TaSUBa; TS. Na. 220/2007)*

Miongozo iliyoorodheshwa hapa chini itatumika kwa Washiriki na wahudhuriaji wote wa Tamasha na itaanza kutumika rasmi kuanzia tarehe ambayo Mwongozo huu umesainiwa kwa pamoja na waliotajwa katika Mwongozo huu.

1. Watoto wote wenye umri chini ya miaka 18 hawaruhusiwi kufanya maonyesho saa za usiku.

2. Pombe au kitu chochote chenye kilevi hakiruhusiwi kuuzwa kwa mtoto mwenye umri chini ya miaka 18 na vilevile ni marufuku kwa mtoto kukubali zawadi yoyote ya aina hiyo. Kitambulisho kinaweza kuhitajika kwa ajili ya uthibitisho.

3. Mtoto lazima aambatane na mzazi au mlezi wake na alindwe ipasavyo. Mtoto yeyote akipatikana na kuonekana kupotea apelekwe kwa Maofisa usalama waliopo.

4. Mbwa anaruhusiwa iwapo ataambatana na mmiliki wake; Kama ni mkali ni lazima adhibitiwe ipasavyo. Uongozi hautakubali kuwajibika kwa namna yoyote kutokana na majeraha au madhara yatakayosababishwa na mbwa kwa mtu yeyote au kwa mbwa mwenyewe.

5. Silaha ya aina yoyote ikiwamo kisu, panga na kifaa kingine chochote cha ncha kali na kilipuzi ni marufuku kuwa navyo katika eneo la Tamasha isipokuwa kwa Maofisa Usalama walioidhinishwa.

6. Mali iliyopotea au kupatikana katika eneo la Tamasha itaripotiwa kwa Maofisa Usalama waliovaa sare. Hata hivyo, Menejimenti haitakubali kuwajibika kwa namna yoyote kwa mali itakayopotea au kuibiwa.

7. Vitendo vyote, mienendo na tabia zote za unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia, vitisho na au kuamsha hisia za kimapenzi ni marufuku katika eneo la Tamasha.

8. Mavazi ya Tamasha inashauriwa kuwa ya kawaida yenye kuzingatia maadili, na mavazi ya kipekee ya ubunifu ya rangi ya hiari isipokuwa kwa mavazi ya maonyesho jukwaani. Ili kuchagua kwa urahisi aina ya mavazi; utabiri wa hali ya hewa katika eneo la Tamasha unaweza kuakisiwa kwa siku na wakati huo mahususi.

9. Hairuhusiwi kufanya biashara na kutumia madawa ya kulevya .

10. Uongozi au waandaaji wa Tamasha hawatawajika kwa namna yoyote kuhusiana na maegesho ya magari au vyombo vyovyote vya usafiri .

11. Mhudhuriaji yeyote haruhusiwi kumshambulia msanii kwenye jukwaa bila kujali kiwango chake cha hasira. Kutunza na kutoa zawadi inaruhusiwa.

12. Matusi na lugha chafu au maneno na tabia ya kuudhi haviruhusiwi.

13. Orodha na Ratiba ya Maonyesho Jukwaani inaweza kubadilika kadiri itavyoonekana inafaa.

14. Msanii haruhusiwi kutumia kilevi au kichocheo chochote cha mwili wakati wa kufanya onyesho lake Jukwaani.

15. Bima ya maisha, afya na mali inashauriwa kwa wasanii wa maonyesho na wahudhuriaji. Menejimenti haitakubali kuwajibika kwa namna yoyote kwa uharibifu wa mali au majeraha kwa mtu yeyote wakati wa Tamasha.

16. Maonyesho ya moja kwa moja jukwaani pamoja na hadhira au yaliyorekodiwa katika picha za mnato au jongefu yanaweza kuchapishwa na kurushwa hewani wakati au baada ya Tamasha.

17. Maonyesho yaliyorekodiwa au makala iliyotayarishwa inaweza kutumika kwa kuzingatia sheria zinazosimamia Hakimiliki na Hakishiriki nchini Tanzania na Mikataba ya Kimataifa iliyoridhiwa.

18. Baada ya kufunga maonyesho ya usiku, wahudhuriaji wote wanashauriwa na kuhimizwa kurejea majumbani mwao au mahali walipofikia.

19. Kila msanii au mhudhuriaji wa Tamasha ana wajibu wa kujiandalia utaratibu wa malazi kwa gharama yake.

20. Vitendo vyote vya uhalifu haviruhusiwai chini ya sheria za Tanzania. Washukiwa wanaweza kupekuliwa, kukamatwa na kufunguliwa mashitaka.

21. Ni lazima kuheshima watu wengine waliohudhuria.

22. Mwenye nia ya kufanya Maonyesho ya Sanaa za Ufundi au kutangaza huduma za taasisi zao na wa kutoa huduma ya chakula na vinywaji ni lazima angalau siku zisizopungua 30 kabla ya tarehe ya Tamasha husika, kuomba na kupata kibali rasmi cha utoaji wa huduma husika ndani ya eneo la Tamasha. Baada ya kuidhinishwa, mwombaji anaweza kutozwa ada au kodi kama itakavyowekwa na Uongozi.

23. Watoa huduma wote walioidhinishwa wanapaswa kutoa huduma zao kwa uhakika katika hali ya usafi.

24. Kila mhudhuriaji anawajibika kwa ulinzi na usalama wa mali zake binafsi. Uongozi hautawajibika kwa hasara yoyote, uharibifu au upotevu wa mali.

25. Takataka zote lazima zitupwe na kuwekwa ipasavyo sehemu inayohusika.

26. Ada ya kiingilio inaweza kupangwa na kutozwa kwa kupewa tiketi. Tiketi iliyopotea haitarejeshwa wala kufidiwa.

27. Wageni wote kutoka nje ya Tanzania wanapaswa kuwa na vibali halali kutoka katika Mamlaka za Serikali zinazohusika.

28. Mtu mwenye magonjwa ya kuambukiza anashauriwa kujitenga kwa hiari yake.

29. Uvutaji sigara lazima uwe katika eneo la pekee au katika eneo maalumu la kuvutia sigara.

30. Ratiba au programu za Tamasha zinaweza kuathiriwa na kitendo au matukio ya asili au yaliyo nje ya uwezo wa Taasisi (majanga yasiyozuilika)

31. Pale itakapotokea kuna hali ya hatari kwa dharura wahudhuriaji wote wanashauriwa kusikiliza na kufuata maelekezo ya wataalamu wa uokoaji.

32. Kuhudhuria kwako katika viwanja vya Tamasha kutachukuliwa na kutafsiriwa kama umekubaliana na masharti ya kupigwa picha, kurekodiwa na kufuata Mwongozo huu.

33. Menejimenti ina uwezo wa kubadilisha au kuboresha Mwongozo huu wakati wowote kadiri itakavyoona inafaa.

| | |
|---|---|
| ……………………………… | ……………………………… |
| GEORGE D. YAMBESI | Dkt. HERBERT F. MAKOYE |
| *Mwenyekiti wa Bodi* | *Mkuu wa Chuo* |

*TaSUBa-Bagamoyo*
26 Januari, 2023